# Ubadilishaji Msimbo kama Mbinu ya Ukwezaji wa Staha Bungeni

Johanes Sylivester Balige

**Ikisiri**

Makala hii inalenga kubainisha jinsi ubadilishaji msimbo unavyotumika katika mijadala ya Bunge la Tanzania kama mbinu ya ukwezaji wa staha. Data za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa nyaraka na ushuhudiaji. Uchambuzi na ufasiri wa data umetumia mkabala wa uchanganuzi kilongo, yaani kufasiri data kwa kuzingatia muktadha wa mazungumzo. Muktadha huo unajumuisha utu, sifa na hadhi ya msikilizaji, kanuni za kitaasisi na kijamii zinazodhibiti majadiliano, mahali pa mazungumzo, urasimi na mada ya mazungumzo. Data za makala hii zinaonesha kuwa ubadilishaji msimbo ni mbinu ya kistaha inayomwezesha mzungumzaji kulinda utu wa viongozi wakuu wa nchi, kupunguza mchomo wa kauli za matusi na kupunguza mchomo wa kauli zinazozungumzia mambo yanayohusu kujamiiana. Hali hii humwezesha mzungumzaji kuepuka kukiuka makatazo ya kijamii na kitaasisi yanayodhibiti mienendo isiyokubalika na hivyo kukweza staha.

## 1.0 Utangulizi

Makala hii ni sehemu ya tafiti mbili zilizofanywa na mwandishi kuhusu matumizi ya lugha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kuanzia sasa BJMT). Utafiti wa kwanza unahusu ubadilishaji msimbo Bungeni na athari zake kwa wasikilizaji (Sylivester, 2011) na utafiti wa pili unahusu uchanganuzi kilongo wa kauli zenye kutweza au kukweza staha katika mijadala ya Bunge la Tanzania (Sylivester, 2016). Lengo kuu la makala hii ni kujadili mchango wa ubadilishaji msimbo katika kukweza staha katika mijadala ya Bunge. Sehemu kubwa ya data za makala hii ilipatikana kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa nyaraka ambapo mtafiti alisoma na kuchambua baadhi ya kumbukumbu rasmi za mijadala ya Bunge za mwaka 1995, 2002, 2004, 2012 na 2013. Kumbukumbu hizi zinapatikana maktaba kuu ya Bunge na kwenye tovuti rasmi ya Bunge. Pia, tulitumia njia ya ushuhudiaji. Hii ilikuwa katika namna tatu: (1) kushuhudia kupitia runinga, (2) kuingia katika ukumbi wa Bunge wakati wa mijadala ya Bunge, na (3) kushuhudia mijadala ya Bunge iliyohifadhiwa katika mfumo wa video. Katika uwasilishaji, uchambuzi na ufasiri wa data tulizozipata katika hansadi, tumeondoa majina halisi ya wazungumzaji tuliowanukuu. Tumetumia herufi za kialfabeti[1] kuwakilisha majina hayo. Makala hii imegawanywa katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inaelezea dhana muhimu ambazo ni staha, kauli zenye kutweza au kukweza staha, na ubadilishaji msimbo, aina na sababu zake. Sehemu ya pili ni mjadala wa kuthibitisha kwa namna gani ubadilishaji msimbo ni mbinu ya ukwezaji wa staha, na sehemu ya tatu ni hitimisho.

[1] Herufi hizo hazina uhusiano na sehemu ya herufi zinazounda jina la Mbunge husika.

## 2.0 Fasili ya Dhana Muhimu

### 2.1 Maana ya Staha

Dhana staha inaweza kujidhihirisha katika mawanda mapana na mawanda finyu (Watts, 2003). Katika mawanda mapana, staha humaanisha tabia na vitendo vyote vinavyofanywa na mtu vyenye kulinda utu wake au utu wa wenzake kwa kuzingatia kanuni na makatazo ya jamii au taasisi inayohusika. Hii inaweza kuwa jinsi anavyovaa, anavyokula, anavyozungumza (mjongeo wa viungo vya mwili), anavyotembea, anavyohusiana na wenzake, na kadhalika. Kwa mfano, kumsalimia mtu anayekuzidi umri au kumpisha akae kwenye kiti huchuliwa kuwa ni matendo ya staha. Katika muktadha wa BJMT, Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2013 Ibara ya 66 zinabainisha mambo kama kusimama kwa utulivu na kubaki kimya wakati Spika anaingia au kutoka Bungeni na wakati Bunge linaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima au katika Kamati ya Matumizi. Matendo mengine ya staha ni kuvaa mavazi ya heshima, kuzima simu, kutopita katikati ya Spika na Mbunge anayesema kutotangatanga kwenye ukumbi wa mikutano. Matendo hayo ya kukweza staha Bungeni pia huhusisha kuinamisha kichwa kuelekea kwa Spika au kufanya mkunjo wa magoti kwa heshima kila mara Mbunge atakapokuwa akienda au kutoka mahali pake. Hata hivyo, kwa kuwa matendo hayo hayahusishi lugha na viashiria vyake hatuwezi kuvichambua kiisimu, hivyo mtazamo huu kuhusu staha hautazingatiwa katika makala hii. Pamoja na hayo, tunakiri kwamba yapo matendo yasiyohusisha lugha yanayoweza kukweza au kutweza staha.

Staha kwa mawanda finyu ni ile inayohusiana na lugha au kwa maneno mengine tunaweza kuiita staha ya kiisimu. Hii hujidhihirisha katika matumizi ya lugha na jinsi yanavyoathiri utu. Mtazamo huu ndio unaohusiana na makala hii na hivyo maelezo na uchambuzi kuhusu staha vitazingatia zaidi mtazamo huu.

Kwa mujibu wa Hill na wenzake (1986) staha ni shurutisho katika mazungumzo ya mwanadamu ambalo lengo lake ni kuzingatia hisia na matakwa ya wengine, kuweka viwango vya kuelewana na kufanikisha mawasiliano. Hii humpa mzungumzaji uchaguzi wa namna mbili yaani ulazima wa mzungumzaji kutambua kanuni zinazoongoza mawasiliano na hiari ya mzungumzaji kuzizingatia. Naye Ayala (2001) anadai kuwa staha ni matendo ya kiisimu ambayo hulinda utu wa msikilizaji. Anaendelea kudai kuwa staha ni mfumo ambao kwao mzungumzaji anaweza kupunguza mchomo kwake au kwa wasikilizaji kwa lengo la kuepuka mgogoro miongoni mwao au kurahisisha mawasiliano katika muktadha wenye hatari ya kusababisha kutoelewana kunakosababishwa na ujumbe wa kauli iliyotolewa.

Kwa hiyo, katika makala hii staha inamaanisha hali inayotokana na matumizi ya mbinu za kiisimu katika mazungumzo ili kuonesha kujali na kuzingatia utu wa mzungumzaji na msikilizaji na kwa kuzingatia kanuni za kijamii na kitaasisi. Hali hii huwezesha mawasiliano na kuepusha migongano na migogoro miongoni mwa wazungumzaji. Mathalani, katika muktadha wa BJMT kanuni zinakataza Mbunge

kumsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yoyote, kutumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine na kutumia lugha isiyo fasaha na ya heshima (taz. kanuni 71 -1(a). Ili kukwepa kuvunja kanuni hizo Mbunge huweza kuteua mbinu faafu za kistaha zitakazomwezesha kukweza staha na hivyo kufanikisha mawasiliano. Hivyo, katika makala hii tunabainisha jinsi ubadilishaji msimbo unavyowawezesha wabunge kutimiza azma hiyo.

### 2.2 Kauli zenye Kutweza au Kukweza Staha

Kauli zenye kutweza au kukweza staha zinaweza kubainishwa kwa kuzingatia mitazamo ya kinadharia ya Grice (1975), Leech (1983), Brown na Levinson (1987) na Fraser (1990).

#### 2.2.1 Mtazamo wa Grice

Kwa mtazamo wa Grice (1975) kauli zenye kutweza staha ni zile zinazoonesha kuwa mzungumzaji hana ushirikiano na msikilizaji wake. Grice anabainisha kuwa tunawasiliana kwa sababu tunashirikiana na ili kushirikiana hatuna budi kuzingatia kanuni ya ushirikiano. Kanuni ya ushirikiano ina vijikanuni vya kiasi (usiseme zaidi ya kinachohitajika), ubora (sema ukweli unaothibitika), uhusiano (sema yanayohusiana na mada tu) na adabu (epuka tungo tata, sema kwa ufupi na pangilia vizuri hoja). Kanuni za Bunge zinaendana na mtazamo wa Grice. Mathalani, kanuni ya 61-(1) inamtaka Mbunge kutosema zaidi ya muda aliopewa kuchangia (kijikanuni cha kiasi), kanuni za 63 (1) na 64-1(a) zinamkataza mbunge kusema uongo (kijikanuni cha ubora) na kanuni ya 64-1(b) inamtaka Mbunge kutozungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala (kijikanuni cha uhusiano). Kwa kuhitimisha, mtazamo wa Grice ni kuwa, kauli yoyote yenye kuvunja vijikanuni hivi ni kauli yenye kutweza staha na wakati kauli yoyote yenye kuzingatia vijikanuni hivi ni kauli yenye kukweza staha.

#### 2.2.2 Mtazamo wa Leech

Kauli zenye kukweza staha kwa mujibu wa Leech (1983) ni zile ambazo ni nzuri kwa msikilizaji. Uzuri wa kauli unapimwa na vijikanuni sita ambavyo kwa ujumla wake vinanuia kumfanya mzungumzaji kuhakikisha kuwa mazungumzo yake yanazingatia kutosababisha maumivu kwa wengine. Vijikanuni hivyo ni umakini (punguza gharama kwa wengine na ongeza faida kwa wengine), ukarimu (punguza faida kwako na ongeza gharama kwako), kukubali (punguza kutowakubali wengine na ongeza kuwakubali wengine), kujisifu (punguza kujisifu na ongeza kutojisifu), maafikiano (punguza kutojiafiki na kutoafikiana na wengine na ongeza kujiafiki na kuafikiana na wengine) na huruma (punguza kutojihurumia na kutowahurumia wengine na ongeza kujihurumia na kuwahurumia wengine). Kimsingi, mawasiliano yanahusisha watu wenye mitazamo tofauti. Kwa hali hiyo, ni vigumu mzungumzaji kumfanya kila msikilizaji wake ajisikie vizuri. Hivyo, mzungumzaji hatakiwi kujikita tu katika kumfanya msikilizaji ajisikie vizuri bali

kuzingatia kanuni zinazoongoza mazungumzo. Mathalani, katika muktadha wa Bunge la vyama vingi lenye makundi yanayotofautiana kiitikadi ni vigumu kumfanya kila Mbunge ajisikie vizuri. Kuna kauli zinaweza kuwafanya upande fulani wajisikie vizuri huku wengine wakijisikia vibaya. Jambo muhimu ni kuzingatia kuwa kauli hiyo haivunji Kanuni za Kudumu za Bunge wala mila na desturi za jamii ya Kitanzania. Pamoja na hayo, katika Kanuni za Kudumu za Mijadala ya Bunge kuna kanuni ambazo zinalenga kumfanya msikilizaji ajisikie vizuri. Kanuni zinakataza kauli za kuudhi, kudhalilisha, uongo na kadhalika.

### 2.2.3 Mtazamo wa Brown na Levinson (1987)

Kwa mtazamo wa Brown na Levinson (1987) kauli zenye kukweza staha ni zile ambazo kwa hakika hulinda utu wa mzungumzaji au msikilizaji kwa kuzingatia uhitaji na matamanio ya mmoja wao. Brown na Levinson wanadai kuwa kauli zinazotolewa na mzungumzaji zinapokuwa kinyume na uhitaji na matamanio ya mzungumzaji au msikilizaji, huitwa kauli zenye kuvunja utu (kutweza staha). Kwa kuwa upo utu wa aina mbili, yaani utu chanya na utu hasi, basi kila aina ina kauli mahususi zenye kuuathiri. Utu chanya unajumuisha matamanio ya mtu ya kupendwa, kukubalika na kuhakikisha kuwa anawashirikisha wengine katika kile akipendacho. Utu hasi ni matamanio aliyonayo mtu ya kutaka kuwa pekepeke ili afanye mambo yake bila kuingiliwa na mtu. Utu ni hali inayoweza kupotezwa, kulindwa au kukuzwa; kwa hiyo, kauli yoyote yenye uwezekano wa kuvunja utu inatakiwa kuepukwa. Kwa kuwa utu unaweza kutwezwa na kwa kuwa washiriki wengi wa mazungumzo wanalinda utu wao kama utaonekana kutwezwa, inachukuliwa kuwa ni raghba ya kila mtu kulinda utu wa mwenzake na kuzungumza kwa namna ambayo kila mtu anaelewa kuwa hili lilikuwa dhumuni lake. Kwa mantiki hii, tuna kauli zenye kutweza staha kwa mtu mwenye utu hasi na kauli zenye kutweza staha kwa mtu mwenye utu chanya.

Kwa mujibu wa Brown na Levinson, utu hasi unaathiriwa mzungumzaji anaposhindwa kuteua kauli zenye kuepuka kuingilia uhuru wa wahusika na hivyo kuathiri uhuru wao wa kuchagua na kutenda. Hii inaweza kumuathiri mzungumzaji au msikilizaji na kusababisha mmoja wao kufuata utashi wa mwenzake. Kwa kufanya hivyo, anakiuka itikadi na mtazamo wake na kufuata mtazamo wa mwenzake.

Kanuni ya msingi ya Nadharia ya Staha kama inavyopendekezwa na Brown na Levinson (1987) ni dhana kuwa, baadhi ya kauli kiasilia huvunja utu na kutweza staha hivyo zinahitaji kupunguzwa makali. Kwa mantiki hiyo, kila wazungumzaji wa lugha fulani huunda mbinu za kiisimu ili kukweza staha lakini wakati huo wakifikia lengo lao la kuwasiliana. Kwa kufanya hivyo, wanapunguza uwezekano wa kuvunja utu ambao ungesababishwa na mazungumzo hayo.

Kimsingi, hoja muhimu ni kuwa, wazungumzaji wanatakiwa kuteua kauli zilizobeba zana za kiisimu zenye kulainisha lugha. Hali hii huondoa msuguano na kuleta mahusiano mema miongoni mwa wazungumzaji na hivyo kufanikisha

mawasiliano. Kwa kuongozwa na mtazamo huu tunabainisha kuwa ubadilishaji msimbo ni mbinu ya kukweza staha bungeni.

### 2.2.4 Mtazamo wa Fraser na Nolen (1981) na Fraser (1990)

Nao Fraser na Nolen (1981) na Fraser (1990) wanadai kuwa kauli zenye kukweza staha ni zile zenye kuzingatia kanuni na masharti ya maafikiano kimazungumzo. Kila jamii au taasisi imejiwekea kanuni na miongozo inayobainisha kauli ipi au uzungumzaji upi unafaa au haufai. Kwa hiyo, kauli yoyote yenye kuzingatia kanuni na miongozo hiyo ni kauli yenye kukweza staha na kauli isiyozingatia kanuni na miongozo hiyo ni kauli yenye kutweza staha. Mtazamo huu unaonekana kuwa na mashiko kwa sababu unatupatia vipengele mahususi vya kutumia kuhukumu kama kauli fulani inakweza au kutweza staha. Mathalani, BJMT lina Kanuni za Kudumu za Mijadala ya Bunge ambazo sharti zizingatiwe. Kanuni hizi zinabeba baadhi ya makatazo yanayopatikana katika mitazamo ya Grice (1975) na Leech (1983).

### 2.2.5 Mtazamo Faafu

Kwa kutilia maanani mitazamo iliyoelezwa hapo juu, tumeamua kuipa umuhimu wa kipekee mitazamo ya Brown na Levinson (1987) na Fraser (1990). Tunachukulia kuwa kauli zenye kukweza staha ni zile zinazolinda utu wa msikilizaji au mzungumzaji. Kipimo cha kuzihukumu ni Kanuni za Kudumu za Bunge pamoja na mila na desturi za Watanzania. Hivyo, ili kuhukumu kuwa kauli inayohusika inatweza au kukweza staha, kwanza, tumezingatia vipengele vinavyopendekezwa na Brown na Levinson, yaani (1) tofauti za kijamii kati ya mzungumzaji na msikilizaji, (2) uhusiano wa kimamlaka kati ya mzungumzaji na msikilizaji, na (3) upangilifu halisi wa masharti katika utamaduni. Pili, sifa za mzungumzaji na/au msikilizaji (anayewasiliana naye) kivyama, kielimu, kiumri, na hali yake ya kisaikolojia, yaani kama amekasirika, amefurahi, mcheshi, mkali, anataka au hataki utani na kadhalika. Tatu, kuwapo kwa wasikilizaji. Nne, Kanuni za Kudumu za Bunge, katiba ya nchi na sheria zinazohusiana na shughuli za Bunge. Vipengele hivi ndivyo vinavyouunda muktadha wa mazungumzo.

## 2.3 Maana ya Ubadilishaji Msimbo

Istilahi hii imeelezwa na wataalamu wengi lakini wafuatao ndio watakaohusishwa katika makala hii. Cromdal (2000) anasema kuwa ubadilishaji msimbo ni matumizi ya lugha mbili au zaidi katika sentensi moja au mfuatano wa sentensi nyingi kati ya watu wawili au zaidi. Hii inamaanisha kwamba, ubadilishaji msimbo hutokea pale tu zaidi ya lugha moja zinapotumiwa katika mazungumzo.

Wataalamu wengine wanasema kuwa, ubadilishaji msimbo ni matumizi ya mbadilishano wa lugha mbili katika jamiilugha uwili ndani ya mada ileile (Grosjean, 1982; Mirloy na Muysken, 1995). Wataalamu hawa wanatumia istilahi ‘ubadilishaji msimbo’ kama istilahi jumuishi ambapo aina tofauti tofauti za

jamiilugha uwili zimejumuishwa. Wanatumia istilahi 'ubadilishaji msimbo ndani' kumaanisha kubadilisha msimbo ndani ya sentensi na ubadilishaji msimbo kati kumaanisha ubadilishaji msimbo kati ya sentensi na sentensi.

Myers-Scotton (1993) pia anatumia istilahi ubadilishaji msimbo kama istilahi jumuishi kwa kuielezea kama matumizi ya lahaja katika mada moja. Wataalamu wengine kama vile Gardnne-Chloros (1991) pia wanasisitiza kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kutokea sio tu kati ya lugha na lugha bali kati ya lahaja moja na nyingine, na pia kati ya namna ya uzungumzaji wa lugha moja.

Minloy na Muysken (1995) kama wanavyofasiliwa na Cromdal (2000) na Grosjean (1982) nao wanasema kuwa ubadilishaji msimbo ni matumizi ya mbadilishano wa lugha mbili au zaidi katika semo ile ile. Maana hii inahusu lugha moja au zaidi ya moja zilizo tofauti. Kwa upande mwingine, Muysken (1995) amepanua maana ya ubadilishaji msimbo kwa kuhusisha vijenzi vya semo ambapo anasema kuwa ni matumizi ya lugha mbili katika semo moja au kirai.

Badala ya kujikita katika kirai au semo, Eastman (1992) anatoa msingi mwingine ambapo anasema kuwa ubadilishaji msimbo ni matumizi ya lugha mbili au zaidi au lahaja za lugha moja kwa kuzingatia uchocheo unaotegemea hali na muktadha wa mazungumzo. Maana hii ni nzuri (tukiachilia mbali dhana ya lahaja za lugha moja) katika makala hii kwani matumizi ya lugha lazima yazingatie muktadha na hali ya mazunguzo. Hii inamaanisha kuwa, uwezo wa mzungumzaji kuwa na umilisi wa lugha mbili unamfanya kuwa na uteuzi wa lugha katika mazungumzo (Kadeghe, 2000). Hata hivyo, uteuzi wa lugha lazima uzingatie muktadha wa mazungumzo unaojumuisha: (1) hadhi na hali ya kisaikolojia ya msemaji na msikilizaji, (2) eneo la mazungumzo (baa, kanisani, Bungeni n.k), (3) aina ya kilongo (majibizano, mahojiano, usaili, hotuba n.k), (4) kanuni za kijamii au kitaasisi, na (5) mada. Jambo hili linabainishwa na Rubin (1968) anayedai kuwa nchini Paragwai ambapo Kihispania na Kiguarani ni lugha rasmi, watu hutumia lugha hizi kwa kuzingatia muktadha wa kijamii. Wazungumzaji hulinda masharti ya kijamii na kiutamaduni. Masharti haya yanajumuisha mfumo wa imani na miiko inayodhibiti tabia za wanajamii na uhusiano wao. Uzingatiaji wa kanuni hizi unawawezesha wanajamii kuwasiliana kwa usahihi.

Katika makala hii tunatumia istilahi ubadilishaji msimbo kama anavyoitumia Cromdal (2000). Anatumia istilahi hii kumaanisha hali ya matumizi ya lugha mbili au zaidi katika tamko moja, au mfuatano wa matamko kati ya wazungumzaji wawili au zaidi. Hii ni maana nzuri ya ubadilishaji msimbo kwa sababu inachukulia ubadilishaji msimbo katika ngazi ya lugha, tofauti na maana nyingine ambazo kama ilivyodokezwa awali zinaangalia ubadilishaji msimbo kati ya lahaja za lugha moja au namna ya uzungumzaji. Kwa kuzingatia maana hii ubadilishaji msimbo ni istilahi jumuishi ambapo inaweza kutokea katika ngazi ya mofimu, neno, kirai, kishazi, sentensi na hata katika ngazi ya kilongo. Jambo la kuzingatia ni kwamba, japo ubadilishaji msimbo huhusisha lugha mbili au zaidi lakini lugha husika hazipotezi sifa zake za kiisimu (Mochiwa, 1979). Hii inamaanisha kuwa,

mifumo ya lugha husika inaweza kuainishwa kirahisi katika kilongo (Maggati, 2004).

### 2.4 Aina za Ubadilishaji Msimbo

Ubadilishaji msimbo hugawanywa katika aina kuu mbili ambazo ni ubadilishaji msimbo ndani na ubadilishaji msimbo kati (Poplack, 1981, 1982; Heller, 1992; Kamwangamalu, 1992).

#### 2.4.1 Ubadilishaji Msimbo Ndani

Istilahi ubadilishaji msimbo ndani hutumika kumaanisha kubadilisha lugha ndani ya sentensi moja (Stephens, 2000). Hapa vipashio katika kiwango cha mofimu, maneno, virai, vishazi na au sentensi kutoka lugha moja, mbili au zaidi vinapatikana ndani au kati ya sentensi (Brice, h.t; Scotton, 1990; Muysken, 2000). Kwa mujibu wa Myers-Scotton (1990), ubadilishaji msimbo ndani ni ubadilishaji wa lugha katika kiwango cha mofimu, neno, kirai au kishazi. Muysken (2000) anabainisha vizuri zaidi kwa kudai kuwa ubadilishaji msimbo ndani ni matumizi ya lugha ambapo vipashio vya kileksika na kisarufi kutoka lugha mbili hujitokeza katika sentensi moja. Katika machapisho mengine aina hii ya ubadilishaji msimbo huitwa uchanganyaji msimbo (Kalong, 2008). Mfano ufuatao unaonesha aina hii ya ubadilishaji msimbo.

**Matini Na. 1**

*Possessive individualism* ya *ku-grab*[2] mali *una-acquire* au unazaliwa nayo? … hapa kila mtu anamwona na anaweza *aji-reform* zaidi kuliko hata yule…wengine *wameji-reform* wengine wanaendelea…kwa mfano, katika nchi kama USA niliwaambia mwaka 1998 ambao *wame-import* kitu kile halafu *waka-export* kitu kile kile…huyu agent NDC *anaji-commit* kwa niaba ya serikali, inayoitwa *National Development Corporation* sasa leo *National Development* inataka kufanya biashara lakini inaingia *in a wrong way inaji-commit* kabisa…

**Chanzo: Kumbukumbu Rasmi za Mijadala ya Bunge: mkutano wa saba Aprili 2002 uk. 54**

Mifano kutoka matini Na. 1 inaonesha jinsi wazungumzaji wanavyobadilisha kutoka lugha moja kwenda nyingine lakini ndani ya sentensi ile ile. Katika matini hii kuna ubadilishaji ulio ndani ya neno, yaani kati ya mofimu na mofimu na ulio ndani ya kirai na pia ndani ya kishazi ambapo viambajengo hivi kwa pamoja vinaunda sentensi.

Mathalani, ubadilishaji msimbo ulio ndani ya neno yaani kati ya mofimu na mofimu upo katika maneno, *ku-grab* (kunyakua), *anaji-reform* (anajibadilisha), *wameji-reform* (wamejibadilisha), *wame-export* (wamesafirisha), *waka-export* (wakasafirisha), *anaji-commit* (anajifunga), na *inaji-commit* (inajifunga). Kimsingi, maneno haya yamekamilika na yanajitegemea kimaana na kimuundo japo

[2] Hati za mlazo ni kama zinavyojitokeza katika hansadi. Msamiati wote wa Kiingereza umeoneshwa kwa hati mlazo.

yameundwa na mofimu za lugha mbili tofauti; za lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Huu ndio huitwa ubadilishaji msimbo ndani ya neno.

### 2.4.2 Ubadilishaji Msimbo Kati

Ubadilishaji msimbo kati humaanisha kubadilisha lugha nje ya mipaka ya sentensi. Hii inamaanisha kuwa matini nzima ya sentensi hutolewa katika lugha moja kabla ya kubadilisha kwenda lugha nyingine katika semo ileile (Myers-Scotton, 1993). Rejea matini ifuatayo:

**Matini Na. 2**

Mheshimiwa Spika, uongozi tunapokezana, leo mimi kesho wewe, kesho kutwa yeye, mtondogoo wao. *I better warn you today comrades*, *you will not afford*. Hatutavumilia matendo batili ya makusudi kwa ajili ya starehe ya watu wachache.

**Chanzo: Kumbukumbu Rasmi za Mijadala ya Bunge: 14 Julai 2004 uk. 82**

Katika matini Na. 2 sentensi "*I better warn you today comrades, you will not afford*" (Ndugu zangu ni vema leo niwatahadharishe, hamtaweza) inaonesha ubadilishaji msimbo kati. Hii ni kwa sababu tungo za Kiswahili zilizopo awali na/au baada yake zinaonekana kuwa nje ya mipaka ya sentensi hizi na zinajitegemea kimuundo na kimaana. Kwa mantiki hii tungo hizi sio sehemu ya sentensi za Kiswahili zilizo karibu nazo. Hivyo basi, huu ndio ubadilishaji msimbo nje ya mipaka ya sentensi uitwao ubadilishaji msimbo kati.

## 2.5 Sababu za Ubadilishaji Msimbo Bungeni

Tafiti kadhaa zimefanyika kuhusu ubadilishaji msimbo na sababu zake kwa ujumla. Hizi ni pamoja na tafiti za Rajabu (1981), Blommaert (1992), Myers-Scotton (1993), Romaine (1996) na Kanyuma (2005). Tafiti hizi kwa ujumla zimejikita katika ubadilishaji msimbo katika mfumo wa elimu kwa mtazamo wa ufundishaji na mbinu za kufundishia.

Katika muktadha wa matumizi ya lugha Bungeni na ubadilishaji msimbo kwa ujumla wataalamu MacWilliam na Chuwa (1990) na Mwansoko na Tumbo-Masabo (1996) wameainisha sababu za ubadilishaji msimbo katika muktadha wa Tanzania. Mathalani, MacWilliam na Chuwa (1990) wanabainisha sababu za ubadilishaji msimbo: Mosi, kujaza pengo lililopo katika msamiati ama wa mzungumzaji mwenyewe ama wa lugha. Pili, kurejea usemi halisi wa mzungumzaji mwingine, au nahau ya lugha nyingine. Tatu, kusisitiza jambo, kutia chumvi au nguvu habari fulani. Nne, kujitambulisha na habari anazozitoa. Tano, kujionesha na kusisitiza umoja wa kundi fulani. Sita, kumtenga mtu mwingine, kujishaua, kujiongezea wadhifa au kuonesha ujuzi. Saba, uvivu au kutojali.

Nao Mwansoko na Tumbo-Masabo (1996) wanasema kuwa ubadilishaji msimbo Bungeni husababishwa na; mosi, kutaka kueleweka au kufahamika. Pili, mazoea. Tatu, kuwapo kwa neno moja la Kiingereza ambalo ni kuntu wakati

hakuna neno moja la Kiswahili na hivyo kulazimika kutumia maneno mengi ya Kiswahili. Nne, upungufu au uchache wa maneno ya Kiswahili yanayotoa dhana inayotakiwa. Tano, kulemaa/ulemavu au kujionesha. Sita, kupata maana kamili ya fikra. Saba, ufafanuzi wa haraka. Nane, kufikiri kwa Kiingereza. Tisa, miswada na maandiko mengine Bungeni kutolewa katika Kiingereza wakati majadiliano huweza kuwa katika lugha ya Kiingereza au Kiswahili. Kumi, jazba. Kumi na moja, kutoa mifano ambayo hueleweka vizuri zaidi kwa Kiingereza. Kumi na mbili, kutojua Kiswahili barabara kunakosababisha ugumu wa kupata maneno. Kumi na tatu, kanuni za Kudumu za Bunge hazimfungi Mbunge asichanganye lugha na kufupisha majadiliano (Wabunge hupewa muda maalumu wa kutoa hoja zao).

Kimsingi, tunakubaliana na hoja zinazotolewa na MacWilliam na Chuwa (1990) na Mwansoko na Tumbo-Masabo (1996) kuhusu sababu za ubadilishaji msimbo Bungeni. Hata hivyo, hawajazingatia kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kujitokeza kwa lengo la kukweza staha. Kwa hiyo, katika makala hii tunabainisha jinsi ubadilishaji msimbo unavyotumika katika mijadala ya Bunge kama mbinu ya ukwezaji staha.

## 3.0 Ubadilishaji Msimbo kama Mbinu ya Ukwezaji Staha

Kama tulivyowanukuu Brown na Levinson (1987) ili kukweza staha, mzungumzaji anatakiwa kuteua mbinu faafu za kistaha. Mbinu hizi zinamwezesha kulinda utu wa mlengwa, makatazo yanayotokana na kanuni za kitaasisi na kijamii zinazoongoza majadiliano. Kwa mtazamo huu kuna wakati ubadilishaji msimbo unajitokeza kwa sababu ya ukwezaji wa staha. Hivyo, sehemu inayofuata inabainisha jinsi ubadilishaji msimbo unavyotumika Bungeni kama mbinu ya ukwezaji wa staha. Mbinu hii humwezesha mzungumzaji kuepuka kuvunja makatazo yanayotokana na muktadha wa mazungumzo (rejea 2.2.5).

### 3.1 Kulinda Utu wa Viongozi Wakuu wa Nchi na Kanuni za Kijamii na Kitaasisi

Kanuni za kudumu za mijadala ya Bunge toleo la 2013 kanuni ya 64(1)(g) inamtaka Mbunge kutotumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine. Pia Kanuni ya 64 (1)(c) inamkataza Mbunge kutomdhihaki Rais. Pia, kwa utamaduni wa kitaifa ni jambo la kustaajabisha mtu yeyote kutamka kauli zenye kuwadhalilisha viongozi wa kitaifa hasa Rais wa nchi. Ili kuepuka kutweza staha mzungumzaji huteua mbinu ya ubadilishaji msimbo ili kupunguza makali ya kauli zake, hivyo kulinda utu wa mlengwa sambamba na kanuni za kitaasisi na kijamii. Rejea matini ifuatayo:

**Matini Na. 3**

**MHE.MBUNGE A:**....Mheshimiwa Waziri Mkuu anampongeza Mheshimiwa Rais kwamba alikwenda sijui kwenye kikao cha G8 *summit* akafika pale, akawasilisha sijui mipango yetu ya kilimo. Kwa hiyo, wanampongeza sana kwa sababu nchi yetu inakwenda kupewa 1.4 *trillion shillings* kukuza *agriculture.* Sasa kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu anajaribu ku-*justify* safari nyingi anazofanya Rais kwamba zile safari zina tija. *It is shameful, how can a father be proud* kwa misaada? *What makes a man proud in this world? It is the money earned out of his effort, out of his knowledge and out of his strength,* siyo msaada.

**Chanzo: Kumbukumbu Rasmi za Mijadala ya Bunge: 26 Juni 2012 uk. 174**

## Muktadha[3] wa Mazungumzo

i. Mzungumzaji A: Mbunge wa chama cha upinzani. Rika la kijana.
ii. Wasikilizaji lengwa: 1. Waziri Mkuu. 2. Rais wa nchi, amiri jeshi mkuu na mwenyekiti wa chama tawala.
iii. Wasikilizaji lengwa wasio wa moja kwa moja ni Wabunge wote wa rika tofautitofauti (vijana, rika la makamo na wazee), hadhi na vyeo mbalimbali, jinsia zote na itikadi (kidini na kisiasa) tofautitofauti.
iv. Wasikilizaji wengineo: Watanzania wa hadhi na rika zote.
v. Mada ya mazungumzo: Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 – Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Katika matini Na. 3, mzungumzaji A anawakosoa na kuwashambulia Waziri Mkuu na Rais wa nchi. Kauli yenye kumkosoa au kumshambulia Rais au Waziri Mkuu isiposukwa vizuri ina uwezekano mkubwa wa kutweza staha. Waziri Mkuu au Rais ni viongozi wa hadhi ya juu hivyo ili kuwakosoa inamhitaji mzungumzaji kutumia busara katika uteuzi wa kauli. Hii itamfanya asivunje Kanuni za Kudumu za Bunge kama vile kanuni ya 64 (1)(g) na 64 (1)(c) kama zilivyonukuliwa hapo juu.

Ili kupunguza mchomo wa kauli zake na ili kuonekana hajavunja Kanuni za Kudumu za Bunge, Mbunge anaamua kuchanganya Kiswahili na Kiingereza. Kauli zilizotamkwa kwa Kiingereza zingeonekana kuwa na mchomo mkali kama zingetamkwa kwa Kiswahili. Mathalani, mzungumzaji anasema:

> *It is shameful, how can a father be proud kwa misaada? What makes a man proud in this world? It is the money earned out of his effort, out of his knowledge and out of his strength, siyo msaada*.
> Ni aibu, baba anawezaje kujivunia misaada? Kitu kinachomfanya mwanamume ajivunie katika dunia hii ni fedha alizozipata kwa jitihada zake, akili zake na nguvu zake, siyo msaada (Tafsiri yetu).

[3] Tumebainisha miktadha ya mazungumzo katika mifano tuliyotoa ili kusaidia kueleweka na ufasiri wa data.

Kimsingi, tafsiri ya Kiswahili inaonesha kuwa na mchomo mkali kuliko ilivyo katika Kiingereza. Mathalani, kauli "baba[4] anawezaje kujivunia misaada?" Inamaanisha mlengwa (Rais wa nchi) anakosa sifa ya ubaba kwa sababu ya kujivunia misaada. Hivyo, hii ni namna laini ya kusema kuwa mlengwa anapwaya katika nafasi aliyopo.

Kama vile haitoshi, anaongezea kauli "ni kitu gani humfanya mwanamume kujivuna katika dunia hii? Ni fedha alizozipata kwa jitihada, akili na nguvu zake, siyo msaada". Katika kauli hii neno 'mwanamume' pamoja na kuwa na maana ya mtu wa jinsia ya kiume, katika muktadha huu (kwa kuzingatia kauli inayofuatia) lina maana ya ziada, yaani mtu anayetumia akili, jitihada na nguvu zake ili kupata mahitaji yake na ya jamii anayoiongoza. Kwa kuzingatia hali hii, kauli hii inamaanisha mlengwa hafai kuwa kiongozi kwani hatumii jitihada, akili na nguvu zake bali anategemea misaada. Ndiyo maana kabla ya kutamka kauli hizi alianza kwa kusema "it is shameful" (ni aibu) kumaanisha mlengwa anajiaibisha, anaaibisha viongozi wenzake, chama chake na taifa kwa ujumla. Kwa kuzingatia kuwa mzungumzaji alikuwa Mbunge wa chama cha upinzani bila shaka alitaka kumaanisha kuwa chama tawala kina viongozi ambao wanaaibisha taifa. Kauli za namna hii zinavunja utu chanya wa mlengwa na wasikilizaji hasa Wabunge wa chama tawala na wananchi wanaompenda kiongozi anayeshambuliwa. Kwa ujumla kauli hizi zinavunja kanuni za 64 (1)(c) na 64 (1)(g) kama zilivyonukuliwa hapo juu. Ili kupunguza mchomo wa kauli hizi mzungumzaji anaamua kutumia mbinu ya ubadilishaji msimbo lakini wakati huo akitimiza nia yake ya kumshutumu au kuweka wazi anaoamini ni udhaifu wa kiongozi husika.

Mzungumzaji anachanganya Kiswahili na Kiingereza kwa kutambua kuwa Bunge linasikilizwa na Watanzania wa hadhi na rika zote. Pia, anatambua kuwa Watanzania wengi hawaelewi Kiingereza. Watafiti mbalimbali kama vile Mekacha (2000), Qorro (2010), na Malekela (2010) wanabainisha kuwa Watanzania wa kiwango cha elimu ya msingi hawaelewi kabisa lugha ya Kiingereza. Kuhusu mijadala ya Bunge inayoendeshwa kwa ubadilishaji msimbo, Sylivester (2011) anadai kuwa takribani asilimia 84 ya Watanzania hawaelewi mijadala ya Bunge inayohusisha ubadilishaji msimbo. Kwa hiyo, Mbunge anapobadilisha msimbo anapotamka kauli yenye kumdhalilisha Rais inakuwa sio rahisi wasikilizaji kung'amua kuwa Rais wao amedhalilishwa na/au utu wake kuvunjwa. Kwa hiyo, uchanganyaji wa Kiingereza na Kiswahili unaweza kupunguza mchomo wa kauli kwa wasikilizaji wengine kwani hawatapata maana halisi ya kauli yenye kuvunja utu wa Kiongozi mkuu wa nchi na kanuni za kijamii na kitaasisi.

### 3.2 Kupunguza Mchomo wa Kauli za Matusi

Katika jamiilugha yoyote kuna kauli ambazo hazitakiwi kutamkwa hadharani kutegemea na muktadha wa mazungumzo. Kauli hizo zinapotamkwa bila

[4] Katika mazingira haya neno baba limetumika kumaanisha kiongozi mkuu wa nchi

kuzingatia muktadha huitwa matusi. Kwa mujibu wa Kamusi ya TUKI (2004) tusi ni neno chafu la kumuudhi mtu. Katika muktadha wa BJMT neno au kauli yoyote chafu na inayomuudhi mtu huchukuliwa kuwa ni tusi. Kwa mujibu wa Mbaya (2002), katika tamaduni za Kiafrika kuna kauli ambazo sio vizuri kuzitamka mbele ya hadhara. Ili kusema alilokusudia mzungumzaji anatakiwa kutumia mbinu faafu ya kistaha. Miongoni mwa mbinu hizo ni matumizi ya tafsida (Mbaya, 2002).

Katika makala hii tunabainisha kuwa ubadilishaji msimbo ni mbinu ya kupunguza mchomo wa kauli za matusi. Hata kama mzungumzaji ana jazba anatakiwa kuzungumza katika namna ambayo hatatukana au kuwadhalilisha wengine. Katika hali ya ubinadamu inaonekana kuna muktadha ambao kuna uwezekano mkubwa wa kujitokeza kauli ya matusi. Hivyo, ili kupunguza mchomo wa tusi hilo, ubadilishaji msimbo hutumika. Rejea matini ifuatayo:

**Matini Na. 4**

**MHE. C:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda nilitaka niwasomee na wananchi waelewe kwamba, wanasema suala la kesi halijatajwa kwenye ripoti yao. Nenda *page* ya nne.
**MBUNGE FULANI:** Mwenendo!
**MHE. C:** *Come on, fuck you!*
**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa C ndiye mwenye nafasi ya kusema. Endelea.
**MHE. C:** Mheshimiwa Naibu Spika, dhidi ya kesi inayomkabili…
**Chanzo: Kumbukumbu Rasmi za Mijadala ya Bunge:17 Aprili 2013 uk. 134**

## Muktadha wa Mazungumzo

i. Mzungumzaji C: Mbunge wa chama tawala, rika lake ni umri wa kati, ana utu hasi.
ii. Kwa upande wa 'Mbunge fulani' pamoja na kuwa hakubainika jina lake ila sauti ilikotokea ni sehemu wanakokaa Wabunge wa kambi rasmi ya upinzani Bungeni. Hivyo, ni Mbunge wa chama kimojawapo cha upinzani.
iii. Wasikilizaji lengwa: Wabunge wa kambi rasmi ya upinzani Bungeni. Wengine ni Wabunge wa vyama vingine. Wabunge wote wana rika tofautitofauti (vijana, rika la makamo na wazee), jinsia zote na dini mbalimbali.
iv. Wasikilizaji wengine: Watanzania wenye hadhi na rika tofauti.
v. Mada ya mazungumzo: Mwongozo wa Spika kuhusu Kuzuia sehemu ya maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Pamoja na kuwa mzungumzaji alikuwa na jazba, inaonekana alibadilisha msimbo kwa kutambua kuwa kauli '*come on, fuck you*' (wewe vipi, mpumbavu) ina mchomo mkali inaposemwa kwa Kiswahili. Pia, tukiangalia kauli za awali, kabla hajakatishwa alinuia kutoa maelezo ambayo yangewafanya wananchi waelewe hoja zake. Kwa hiyo, ghafla anapotaka kutoa tusi anaamua kubadilisha lugha ili

wananchi wasimuelewe. Kwa kufanya hivyo inasaidia kupunguza mchomo wa kauli. Kama tulivyosema awali, Kanuni za kudumu za mijadala ya Bunge toleo la 2013 kanuni ya 64(1)(g) inamtaka Mbunge kutotumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine. Kwa kutambua hali hii mzungumzaji anatumia ubadilishaji msimbo kama mbinu ya kukweza staha. Hili linajidhihirisha tunapoona Kiti kinamruhusu bila kumtaka kufuta kauli jambo ambalo labda lisingejitokeza iwapo mzungumzaji angetoa kauli hiyo kwa Kiswahili.

### 3.3 Kupunguza Mchomo wa Mambo Yanayohusu Kujamiiana

Kwa mujibu wa Mbaya (2002) katika jamii za Kiafrika maneno ambayo ni mwiko kuyatamka hadharani ni pamoja na maneno yanayohusu sehemu za siri (hasa viungo vya uzazi) na shughuli zinazofanywa na viungo hivyo. Jambo fulani likishabainishwa kuwa ni mwiko halitakiwi kutamkwa, kufanywa, kuguswa au kuangaliwa (Madu, 2002). Mbaya (keshatajwa) anadai kuwa njia mbadala ya kutamka maneno hayo ni kutumia tasfida. Pamoja na kuwa tunakubaliana na matumizi ya tasfida kama mbinu ya kupunguza mchomo wa kauli zinazotweza staha, katika makala hii tunabainisha kuwa mbinu nyingine ni matumizi ya ubadilishaji msimbo. Rejea matini ifuatayo:

**Matini Na. 5**

**MBUNGE C:** …tuelimishane, lakini yeyote ambaye atakuwa anabagua wanafunzi kijinsia na kuwaondoa watoto kwenda kuolewa, apewe adhabu kali na tuelimishe watu kama tulivyoelimisha katika mambo ya *sex* ya UKIMWI (Kicheko/makofi).

**Chanzo: Kumbukumbu Rasmi za Mijadala ya Bunge: 24, Aprili 1995 uk 525**

### Muktadha wa Mazungumzo

i. Mzungumzaji C: Mbunge wa chama tawala, rika lake ni umri wa makamo, ana utu chanya.
ii. Mlengwa: Waziri wa Elimu na Utamaduni.
iii. Wasikilizaji lengwa: Wabunge wote wa rika tofautitofauti (vijana, rika la makamo na wazee), jinsia zote na dini mbalimbali.
iv. Mada ya mazungumzo: Hoja ya Wizara ya Elimu juu ya kurekebisha sheria.

Katika matini hii, mzungumzaji kwa kutambua kuwa kutamka hadharani mambo yanayohusu kujamiiana kunatweza staha anaamua kutumia ubadilishaji msimbo kama mbinu ya kupunguza makali ya kauli yake. Matumizi ya neno “*sex*” (ngono) yamepunguza au kuondoa uwezekano wa Mbunge kutamka mambo ya aibu hadharani. Hata katika mazungumzo ya kawaida ni rahisi mzungumzaji kutaja viungo vya uzazi kwa kuchomekea Kiingereza katika mazungumzo yake. Hii inamaanisha kuwa ubadilishaji msimbo, kwa kiasi fulani, ni mbadala wa matumizi ya tasfida.

## 4.0 Hitimisho

Ubadilishaji msimbo sio matumizi ya lugha yenye kujitokeza kwa bahati mbaya bali ni mojawapo ya mbinu ya kimawasiliano yenye lengo maalumu kutegemeana na muktadha (Shin & Milroy, 2000; Shin, 2010; Shartiely, 2013). Kwa hiyo, data ya makala hii inaonesha kuwa pamoja na ubadilishaji msimbo kutokea kwa sababu zinazotolewa na Macwiliam na Chuwa (1990) pamoja na Mwansoko na Tumbo-Masabo (1996) kama tulivyozibainisha awali, kukweza staha ni sababu nyingine inayochochea uzungumzaji wa namna hii. Kwa kutambua kuwa Watanzania wengi hawaelewi kauli zenye kuhusisha ubadilishaji msimbo (Sylivester, 2011) mzungumzaji anapoona kuna uwezekano mkubwa wa anachotaka kuzungumza kutweza staha kwa kuvunja utu wake au wa msikilizaji na/au kuvunja Kanuni za Kudumu za Bunge anaamua kutumia ubadilishaji msimbo. Kwa hiyo, pale Mbunge anapoona hakuna uwezekano wa kuepuka kutoa kauli anayotaka kuitoa, ni bora kuteua mbinu faafu itakayopunguza mchomo wa kauli inayohusika. Mbinu mojawapo ni ubadilishaji msimbo.

**Marejeleo**

Ayala S. P. (2001). "FTAs and Erskine May: Conflicting needs?- Politeness in Question Time" katika *Journal of Pragmatics* 33: 143-169.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2007). *Kanuni za Kudumu za Bunge*. Toleo la 2007.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania . (2013). *Kanuni za Kudumu za Bunge*. Toleo la Aprili, 2013.

Brice, A. (2000). "Code Switching in the ESL Classroom, A Study of Pragmatic and Syntactic Features, Advances in Speech Language Pathology", katika *Journal of the Speech Pathology Association of Australia*, 1(20): 19-28.

Brown, P. na Levinson. S. (1987). *Politeness: Some Universals in Language Usage*. Cambridge: Cambridge University Press.

Cromdal, J. (2000). *Code Switching for All Practical Purposes, Bilingual Organization of Children's Play*. New York: St Mattin's Press Inc.

Fraser, B. (1990). "Perspectives on Politeness" katika *Journal of Pragmatics* 14(2):219-236.

________ (1975). *The Concept of Politeness*, Paper Presented at the 1985 NWAVE Meeting, Georgetown University.

Fraser, B. na Nolen W. (1981). "The Association of Deference with Linguistic Form" katika *International Journal of the Sociology of Language* 27: 93-109.

Gardnne-Chloros, P. (1991). *Social Development of Linguistic Change in Bilingual Austria*. New York: Academic Press.

Grice, H. P. (1975). "Logic and Conversation" katika Cole, P na Morgan, J. (wahariri), *Syntax and Semantics* 3, New York: Academic Press, kur. 41-58.

Grosjean, F. (1982). *Life With Two Languages, An Introduction to Bilingualism*. London: Harvard University Press.

Hill, B., Ide, S., Ikuta, S., Kawasaki, A. & Ogino, T. (1986). "Universals of Linguistic Politeness: Qualitative Evidence from Japanese and American English", katika *Journal of Pragmatics*, 10 (3):347-371.

Kadeghe, M. (2000). The Implication of Bilingualism in Learning and Teaching: The Case of Tanzania Secondary Schools, Dar es Salaam. Doctorial Thesis (Haijachapishwa), University of Dar es Salaam.

Kanyuma, Y. (2005). Social Motivations for Code-Switching Among Members of Primary School Communities: A Case Study of Rubour Ward, Tarime District, M.A Dissertation (Haijachapishwa), University of Dar es Salaam.

Lakoff, R. (1990). *Talking Power*. New York: Basic Books.

Leech, G. (1983). *Principles of Pragmatics*. London: Longman.

Levinson, S. C (1983). *Pragmatics*. Cambridge: Cambridge University Press.

MacWilliam, A. na Chuwa, A. (1990). "Kubadili Msimbo Bungeni" katika *Kiswahili Juzuu* 57, Dar es Salaam: TUKI, kur. 33-45.

Madu, S. N. (2002). "Health Complaints of High School Students in the Northern Province and Taboo Themes in Their Families" katika *South African Journal of Education*, 22(1):65-69.

Maggati, C. (2004). The Influence of Kiswahili on Non-Bantu Languages: The Case of Dholuo in Tarime, M.A Dissertation (Haijachapishwa), University of Dar es Salaam.

Malekela, G. A. (2010). English as a Medium of Instruction in Post-Primary Education in Tanzania: Is it a Fair Policy to the Learners? Katika Brock-Utne, B., Desai, Z., Qorro, M., A. S., & Pitman, A. (Wah.) *Language of Instruction in Tanzania and South Africa*. Boston: Sense Publishers. kur. 33-42.

Mbaya, M. (2002). "Linguistic Taboo in African Marriage Context: A Study of the Oromo Laguu*"* katika *Nordic Journal of African Studies*, 11(2): 224-235.

Mekacha, R.D.K. (2000). *Isimujamii*. Osaka: Osaka University.

Mirloy, L. na Muysken, P. (1995). *One Speaker, Two Languages, Cross Disciplinary Perspective on Code Switching*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mochiwa, Z.S.M. (1979). The Impact of Kiswahili Language on Ethnic Languages: A Case Study From Handeni Disrict. M.A Dissertation (Haichapishwa), University of Dar es Salaam

Muysken, P. (2000). *Bilingual Speech, A Typology of Code-mixing*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mwansoko, H.J.M. na Tumbo-Masabo, Z.N.Z. (1996). *Matumizi ya Kiswahili Bungeni*, Dar es Salaam: TUKI.

Myers-Scotton, C. (1983) "The Negation of Identities in Conversation*:* A Theory of Markedness and Code Choice", in *International Journal of the Sociology of Language*.

Poplack, S. Sankoff, D. and Miller, C. (1988). "The social Correlates and Linguistic Processes of Lexical Borrowing and Assimilation", katika *Linguistics* 26:. 47-104.

Qorro, M. (2010). Testing Students' Ability to Learn through English during the Transition from Primary to Secondary Schooling. Katika Brock-Utne, B., Desai, Z., Qorro, M., A. S., & Pitman, A. (Wah.) *Language of Instruction in Tanzania and South Africa*. Boston: Sense Publishers. kur. 157-188.

Shartiely, N. E. (2013). Discourse Strategies of Lecturers in Higher Education Classroom Interaction: A Case at the University of Dar es Salaam Tanzania, PhD Dissertation, Stellenbosch University.

Shin, S.Y. (2010). "The Functions of Code-Switching in a Korean Sunday School" katika *Heritage Language Journal* 7 (1):91-116.

Shin, S.J. na Milroy, L. (2000). "Conversational Code Switching among Korean-English Bilingual Children" katika *International Journal of Bilingualism*, 4(3):351-383.

Sylivester, J. (2011). Ubadilishaji Msimbo Bungeni na Athari Zake kwa Wasikilizaji. Tasinifu ya M.A Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Watts, R. (2003). *Politeness*. Cambridge: Cambridge University Press.

________(1992). "Linguistic Politeness and Politic Verbal Behavior: Reconsidering Claims for Universality" katika: Richard J. Watts, K. Ehlich and S. Ide, (wahariri) *Politeness in language: Studies in its History, Theory and Practice*, Berlin: Mouton de Gruyter, kur. 109-129.

William, F. (1997). *Anthropological Linguistics: An Introduction*. Massachusetts: Blackwell Publishers Inc.

Wu, Y. (1985). "Code-Mixing by English-Chinese Bilingual Teachers of the People's Republic of China", *Journal of World Englishes*, 4(3):303-317.